

Ni vizuri kujua haya

By SW - Melkisedeck Shine · April 11, 2015

Biashara - Mbinu za Ujasiriamali na Biashara Kufanya tofauti · #Karibu AckySHINE · #SMS, Vichekesho, Mahusiano, Biashara na Ujasiriamali, Afya, Chemsha Bongo, Dini pamoja na Vitabu kwenye PDF · #Ujasiriamali: Kujitambua na Kuwa na Mafanikio Katika Maisha · #Ujasiriamali: Matumizi ya Fedha · #Ujasiriamali: Mbinu za Kuwa Tajiri

??Degree au vyeti ulivyo navyo haviwezi kukupa mafanikio. ??Uzuri ulio nao hauwezi kukupeleka kwenye ndoto zako. ??Usipobadilisha hao marafiki ulio nao hutofika mahali popote.

??Usipobadilisha vitendo unavyovifanya kila siku hivyo hivyo mafanikio utayasikia kwa wengine.

??Kazi au ajira unayoifanya usipojiongeza haiwezi kukupeleka kwenye maisha unayoyataka.

??Huo mshahara unaolipwa usipoutumia vizuri na kujiwekea akiba au kuwekeza kidogokidogo hutoacha kulalamika kila siku mshahara mdogo au hautoshi.

??Usipoacha kukopa bila malengo mafanikio ni ngumu kuyapata.

??Usipowekeza muda kwa ajili ya kujifunza na kuelewa mambo mengi ya biashara na ujasiriamali kwa ujumla na kufahamu dunia imetoka wapi,iko wapi na inaelekea wapi huytoacha kulalamika.

??Usipolipia gharama za kujifunza na ukajifunza kweli kile unachoelekezwa ikiwa ni pamoja na Pesa na muda haya mambo waachie wengine.

??Usipobadili fikra na mtazamo wako huwezi kubadilisha chochote katika maisha yako.

??Ukiacha kusikiliza kila aina ya ushauri unaopewa na ndugu zako,jamaa zako,marafiki zako,familia yako,majirani zako na kujisikiliza wewe mwenyewe utahangaika sana.

??Usipofanya bidii na juhudi na ukakubaliana na changamoto zozote utakazokutana nazo maisha yatakuwa magumu sana kwako.

Kumbuka mtu pekee Wa kuyabadilisha maisha yako na kukusaidia kufikia malengo na ndoto zako wala sio mwingine ni mmoja tu nae ni WEWE. Badilisha fikra zako,badilisha mtizamo wako,badilisha maisha yako.